

Risala iliyotangulia kusomwa na Mlezi wa Kwaya Kuu Mama Elipina Mlaki

Mpendwa Baba Mchungaji,

Wapendwa Washarika, Marafiki na wanakwaya kwa ujumla.

KWAYA KUU - Kwaya ya Usharika Kanisa Kuu Azania Front ikiwa chini ya KKKT Dayosisi ya Mashariki na Pwani (DMP), ni Kwaya kongwe katika kwaya kuu nyingi za Dayosisi ya Mashariki na Pwani. Kwaya kuu ilianza zaidi ya miaka 64 iliyopita. Hadi sasa ina waimbaji 60 walioandikisha, ingawaje mahudhurio ya kila ibada ni kati ya 30 na 40.

Kwaya hii ni mionganini mwa vikundi vinavyofanya vizuri hadi sasa katika matukio mbalimbali ya Usharika, na nje ya Usharika na hata mwaka jana Kwaya Kuu ilikuwa mshindi wa kwanza wa Dayosisi yetu.

Katika matukio makuu yaliyoleta historia au kujulikana kwa kwaya hii, ni uimbaji wao wa kuimba kwa kinanda au kuimba bila vyombo kwa utaalamu.

Nachukua nafasi hii kwa niaba ya Kwaya Kuu kuwakaribisha wote tushiriki katika furaha ya uzinduzi wa Audio CD vol. ya 9 ya kwaya Kuu.

Wameniomba niseme machache ya shukrani kabla ya kuanza kununua hizi CD.

Wanapenda kuwashukuru wote kwa ushirikiano mzima kuanzia maandalizi hasa kwa uongozi wa usharika kuwapa nafasi hii ya kuzindua Audio CD hii vol 9 inayoitwa SIKU MMOJA.

Ombi lao kwenu muwaunge mkono kuzinunua ili maandiko yatimie. Neno la Mungu lienezwe kila mahali.

Kwaya kuu ina mipango ya muda mrefu na ya muda mfupi, kutokana na muda hatutaweza kuitaja yote hapa, ila michache ni:

- **Kuungeza kiwango cha uimbaji ikiwa ni pamoja na semina za uimbaji na kulipia gharama za wataalamu wa muziki.**

- *Wanataka kununua sare za kikundi;*
- *Wangependa wa record DVD;*
- *Kuendeleza ushirikiano ndani na nje ya mipaka yetu na ikimpendeza Mungu wawe na usafiri wao utakaowawezesha kwenye shughuli za uinjilisti, na kuwa na kitega uchumi cha kikundi.*

Ndugu washarika na marafiki wote mlioalikwa leo nimalizie kwa kuwakaribisha kuungana na kwaya kuu ili lengo la kueneza neno la Mungu litimie.

Kwaya Kuu inafanya mazoezi mara mbili kwa wiki, yaani JUMANNE na IJUMAA, ina Walimu wazuri karibuni sana mjiunge na kwaya.

ASANTENI SANA